JENGA DARAJA

Mahubiri ya Neno la Mungu

Kimeandikwa na
Mchg. Bent H. Joergensen

SOMA BIBLIA

YALIYOMO

Utangulizi 5

I Kwa Nini Tuhubiri? 7
(a) Tumeagizwa na Mungu 7
(b) Hatuwezi Kunyamaza 8
(c) Mahitaji ya Watu 10
1. Mahitaji ya Wasio Wakristo 10
2. Mahitaji ya Walio Wakristo 11

II Tuhubiri Nini? 13
(a) Asili na Maana ya Neno "Kuhubiri" 14
(b) Ujumbe wa Mahubiri 14
1. Tumhubiri Kristo 14
2. Msalaba Uwe Kiini cha Mahubiri 15
(c) Hitaji la Kuifahamu Biblia Yako 17

III Jinsi ya Kuandaa Mahubiri 19
(a) Hitaji la Kujiandaa 19
(b) Tafuta Mapema Neno la Mahubiri 20
(c) Kupanga Muda, Mahali na Vifaa vya Maandalizi 21
1. Andaa Mapema! 21
2. Tafuta Mahali Penye Utulivu na Faragha 21
3. Kifaa Kinachoweza Kukusaidia 22
(d) Msingi wa Maandalizi 23
1. Maombi na Utakaso 23
2. Kufunga 24
(e) Maandalizi ya Mahubiri Yenyewe 25
1. Kutafakari 27
2. Kupanga Hatua za Mahubiri 37
3. Kuandika Mahubiri Yenyewe 42

IV Jinsi ya kupata Wokovu 45
(a) Kumjua Mungu Alivyo 45
1. Mungu Alivyojifunua 45
2. Kuzuia Kudanganywa na Shetani 49
3. Kunena kama Lilivyoandikwa 50

(b) Jinsi ya Kupambanua Utakatifu wa Mungu na Upendo wa Mungu katika Biblia 52
1. Mifano ya Agano la Kale 52
2. Mifano ya Agano Jipya 55
3. Kujumlisha 60
(c) Mungu Anavyomwokoa Mwanadamu kwa Neno Lake 61
1. Mfano wa Shamba na Mbegu 61
2. Kazi ya Sheria 61
3. Kazi ya Injili 62
4. Kazi ya Sheria na Injili Katika Maisha ya Mtu Aliyeokoka Tayari 63
Nyongeza 66
Muhtasari juu ya Jinsi ya Kupata Wokovu 66
Baadhi ya Machapisho Yenye Miongozo ya Kujisomea Biblia kwa Utaratibu 67
Vitabu vingine kutoka Soma Biblia 68

UTANGULIZI

Ndugu msomaji, karibu kujifunza habari ya kitabu hiki. Ujengaji wa daraja ni jambo tunalofahamu sana katika mazingira yetu ya Tanzania. Kuna madaraja ya aina nyingi. Madaraja mengine ni makubwa na ya kudumu ambayo yametengenezwa na wataalamu kwa mfano kwenye barabara kuu itokayo Dar es Salaam hadi Tunduma au kwenye reli ya Tazara. Mengine yametengenezwa na wenyeji ambayo siyo ya kudumu. Daraja linaweza likawa la ubao mmoja tu uliowekwa juu ya kijito ili watu wanaotembea kwa miguu waweze kuvuka. Hata hivyo madaraja yote ya kila aina yana lengo moja tu ambalo ni kuwezesha watu kuvuka au kuvusha vitu kutoka ng'ambo moja hadi ng'ambo nyingine. Maana ng'ambo moja imetengwa na ng'ambo nyingine kwa sababu ya mto au korongo fulani. Bila daraja hakuna uwezekano wa kuvuka. Na kama kuna mtu ambaye angetaka kuvuka bila daraja kuvuka kwake kungekuwa kwa taabu sana, au bila uwezekano kabisa.

Nakumbuka siku moja tulipanga kwenda katika kijiji kimoja ili kuhubiri Neno la Mungu na kufanya uinjilisti. Njiani kulikuwa na daraja ambalo ni lazima gari lipite juu yake. Hapakuwa na njia yo yote nyingine ya kuvuka mto ule. Kwa bahati mbaya baadhi ya mbao kwenye daraja hilo zilikuwa zimechukuliwa na watu. Basi, tulikuwa na njia moja tu: tulitengeneze daraja! Haya, tukatafuta mbao na kulitengeneza. Ndipo tukavuka, na ujumbe wa Mungu ukawafikia watu wa kijiji kile.

Kuhubiri ni kama kujenga daraja. Ni kujenga daraja kutoka hilo somo lililoandikwa miaka mingi iliyopita mpaka watu wa leo nao wajitambue: "Kumbe! somo hili lina maana hii na lina ujumbe hata kwangu mimi leo!" Mahubiri yanahitajika kama daraja kutoka Neno la Mungu (yaani kutoka kwa Mungu) mpaka mioyo ya wasikilizaji, ili hilo Neno la Mungu lipate kukaa mioyoni mwao na kuyabadilisha maisha yao. Ng'ambo moja ni Biblia na ng'ambo nyingine ni watu. Katikati kuna korongo ambalo ni watu kutokujua, kutokuelewa au kutokupokea ujumbe wa Mungu. Kwa hiyo ujumbe unahitaji kuvushwa. Mahubiri ndiyo daraja la kuvushia ujumbe. Kwa hiyo ninaposema "Jenga daraja!" maana yake ni "Hubiri Neno la Mungu!".

"Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri?" Rum 10:13-14. Uliyepata wito wa kulihubiri Neno la Mungu umepata wito muhimu sana na pia mgumu sana. Mungu akubariki!

Katika kitabu hiki sijagusia kila aina ya mahubiri. Katika sehemu ya I, ya II na ya IV nimeandika juu ya mambo ya msingi kwa mahubiri yo yote yale, lakini katika sehemu ya III nimefikiria hasa aina moja ya mahubiri. Ni mahubiri yale ambayo yanatakiwa kutolewa kanisani kila Jumapili kufuatana na neno maalumu, ambalo limepangwa katika kalenda ya kanisa. Ni matumaini yangu na ombi langu kwamba mafundisho ya kitabu hiki yapate kukusaidia na kukuongoza katika wito wako muhimu. Mungu akusaidie!

I

KWA NINI TUHUBIRI?

Inawezekana wengine wanahubiri ili waonekane na watu. Huenda yanajitokeza mawazo kama haya yafuatayo: Mimi najulikana! Mimi nasimama mbele ya watu! Mimi ni mtu! Au pengine wengine wanahubiri kwa sababu ya kumsema mtu au kuwasema watu katika mambo fulani. Huenda unaweza kupata mawazo yafuatayo: "Kumbe, mtu huyu hataki kunisikia! Haya, tutaona Jumapili!"

Sababu hizo si halali mbele za Mungu bali ni kinyume. Bila shaka wahubiri wengi wamewahi kujaribiwa katika mambo kama haya. Kwa mfano kutaka kuonekana mwenyewe badala ya kumfanya Yesu aonekane. Lakini sasa tuangalie sababu zinazofaa katika kuhubiri Neno takatifu la Mungu.

(a) Tumeagizwa na Mungu

Yesu Kristo ameagiza: "Enendeni ulimwenguni mwote, *mkaihubiri* Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa." Mk 16:15-16. Agizo hili analitoa Yesu kutokana na shauri maalumu alilokata Mungu: "Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, *Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa*." 1 Kor 1:21. Kwa hiyo ni wazi kwamba njia maalumu Mungu aliyoichagua ili kueneza Ufalme wake hapa duniani na kuwaokoa wanadamu ni njia ya *mahubiri ya Neno lake!*

Kumbuka pia maneno ya Rum 10:17: "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja *kwa neno la Kristo*". Kabla ya neno hili kuna maswali fulani muhimu yanayoulizwa katika mstari 13-15: "... kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? *Tena wamsikieje pasipo mhubiri?* Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, *Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari njema!"*

Hii ndiyo sababu ya msingi ya kuhubiri: Mungu mwenyewe amekata shauri na kuagiza iwe hivyo! Na shauri la Mungu sisi hatuwezi kubadili wala kufuta. Mahubiri ya Neno la Mungu yameanzishwa moyoni mwa Mungu mwenyewe. Kujua hivyo kunatutia nguvu na ujasiri sana tunaposimama mimbarani: *Mungu* ndiye aliyeagiza, kwa hiyo *Mungu mwenyewe* yupo pamoja nasi katika kazi hii! Na tukiangalia matokeo mbali mbali ya mahubiri ya Neno la Mungu tunahakikishiwa na kutambua wazi kuwa kweli Mungu ameamua hivyo. Maajabu mengi yanafanyika!

Mfano mmoja ni matokeo ya mahubiri ya Mtume Petro siku ya Pentekoste: Mdo 2:36-41. Watu walichomwa mioyo yao, na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu waliobatizwa na kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Mifano mingine: Mdo 10:34-48; 13:44-48; 16:13-15 na 17:32-34.

Mfano wa siku hizi: Tupo katika mji mmoja wa Tanzania. Mzee mmoja ameingia kanisani ili kuhudhuria mkutano wa kiroho. Anaposikiliza mahubiri hajisikii raha. Neno la Mungu linamchoma moyoni mwake. Wiki iliyopita alibishana na rafiki yake. Rafiki yake ndiye aliyekosa, na aliondoka kwake kwa hasira. Sasa anapokaa kanisani na kusikiliza Neno la Mungu hana raha. Na mwisho inambidi atubu moyoni mwake na kukiri hasira yake mbele ya Mungu. Inambidi amsamehe rafiki yake. Na mkutano ulipokwisha ikabidi amtafute rafiki yake na kupatana naye. - Basi, tunaona tena ukweli wa neno hili: "... Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa"!

Kutokana na shauri hili la Mungu, kuna Wakristo maalumu anaowapa wito na kipawa cha kuhubiri. Wito huu huwa unathibitishwa na kanisa linapotoa wito kwa Wakristo fulani kuwa wahubiri. Angalia mfano wa Mtume Paulo: Mdo 13:1-5. Na tukiangalia kwa upande wa karama za Roho Mtakatifu tunaona kwamba miongoni mwa karama nyingi, moja wapo ni karama ya kuhutubu! Angalia 1 Kor 14 (hasa mstari wa 1-5, 19 na 23-25).

(b) Hatuwezi Kunyamaza

Mtume Petro na Mtume Yohana wanashuhudia: "sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia." Mdo 4:20. Na Yohana anaendelea katika barua yake: "hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na

ninyi." 1 Yoh 1:3. Yaani hawawezi kunyamaza. Wameona mambo makuu ya ajabu ambayo lazima wawashirikishe na wengine. Ni *mashahidi.* Huyu Yesu Kristo wanayemhubiri, wao wenyewe wamemwona na kumpokea na kumpenda. Roho Mtakatifu amemiminwa katika mioyo yao, kwa hiyo kuna msukumo wa ndani wa kushuhudia na kuhubiri.

Ni kama yaliyotokea katika kijiji kimoja kilichoitwa Majihaba. Ilikuwa wakati wa kiangazi na ukame ulikuwa mkubwa mwaka ule. Visima vyote vilikauka kabisa. Kwa kweli watu walipata shida sana kwa maana mto ulikuwa upo mbali sana. Siku moja baba mmoja alikwenda msituni kutafuta kuni si mbali sana na kijiji cha Majihaba. Akiwa msituni akagundua chemchemi ya maji ambayo walikuwa hawajawahi kuiona. Akafurahi kweli moyoni mwake na akaweka alama ili aweze kuiaona tena. Ilikuwa ni kwenye miamba fulani chini ya mizizi ya mti mkubwa.

Basi, akarudi kijijini kwa mbio. Je, unafikiri aliweza kunyamaza kimya aliporudi kijijini? Bila shaka alimwambia kila mmoja aliyekutana naye habari ya hiyo chemchemi mpya, na baada ya muda mfupi watu wote wa kijiji cha Majihaba walijua habari hiyo. Wakacheka na kufurahi na wakamwomba huyu baba awaonyeshe mahali penyewe. Huyo baba alikuwa shahidi na kila mmoja aliyepata kupaona akawa shahidi pia.

Sababu hizi zote mbili (a na b) ni muhimu sana. Kwanza mahubiri yako hayatakuwa na nguvu na ukweli ndani yake kama hujaliamini na kulipokea wewe mwenyewe Neno unalohubiri. Ni kama mwanakijiji mmoja wa Majihaba ambaye alimwambia jirani yake kwamba kuna chemchemi moja nzuri sana msituni, lakini jirani yake alipomwomba amwonyeshe hiyo chemchemi akashindwa, kwa maana alikuwa bado hajaiona yeye mwenyewe, alikuwa amesikia tu!

Pili ni muhimu sana kwako kujua kwamba unahubiri kwa sababu umetumwa na *Mungu* kuhubiri, hujajituma mwenyewe. Wakristo wote wanatakiwa kumshuhudia Kristo kwa wengine, lakini si wote wanaopata wito wa *kuhubiri*.

Kama kweli wewe umeitwa na Yesu kuhubiri na pia ni shahidi, hakika mahubiri yako yatakuwa na matokeo mema! Neno la Mungu linashuhudia hivyo kama tulivyoona!

(c) Mahitaji ya Watu

Kwa nini tuhubiri? Kwa sababu tumeagizwa na Mungu na hatuwezi kunyamaza. Jambo la tatu: Watu wanahitaji mahubiri yetu. Bila mahubiri hawapati mawasiliano mazuri na Neno la Mungu, hawapati msaada ambao Mungu anapenda kuwapa. Mahitaji ya watu ni tofauti. Kimsingi kuna makundi mawili yenye mahitaji tofauti.

1. Mahitaji ya Wasio Wakristo

Jambo hili tulishaona katika lile neno la Rum 10:13-17. Hebu lisome neno hilo tena! Neno lingine ni lile la Mk 16:15-16: "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*" Angalia pia 2 Pet 3:9. - Mahitaji ya wasio Wakristo ni kupata wokovu katika Yesu Kristo *ili wasipotee!* Hiyo haitawezekana bila mahubiri ya Neno la Mungu.

Nakumbuka mfano wa kijana mmoja katika eneo la misioni nilipokuwa ninafanya kazi. Mwinjilisti wa mahali pale alijitahidi sana kuwazuru watu nyumba kwa nyumba akiwahubiria Habari Njema. Basi, katika eneo moja kulikuwa na vijana watano ambao waliamua kumpokea Yesu na kubatizwa. Hii ilikuwa ni furaha kubwa. Lakini yaliyotokea baadaye ni kwamba mmoja wao akafariki kwa sababu ya ugonjwa fulani. Tena mwaka ulikuwa haujaisha tangu abatizwe. Faraja yetu ni kwamba huyu kijana alipata kuokoka kabla hajafa. Akazikwa Kikristo na tegemeo letu ni kwamba amekwenda Mbinguni. Shukrani kwa Mungu! Na hayo yote ni kwa sababu huyo mwinjilisti alikuwa tayari kutumwa na Mungu kuhubiri Habari Njema. La sivyo huyo kijana angalipotea.

2. Mahitaji ya Walio Wakristo

Mti usiokua tena umekufa. Matokeo yake ni kukauka kwa huo mti. Kukua ni dalili ya uhai. Hata mtoto asipoendelea kukua na kuongezeka mwili ni hatari. Mkristo anahitaji kukua katika imani. Anahitaji kumfahamu Mwokozi wake zaidi na zaidi. Bila hivyo uhai wake wa kiroho utafifia na baadaye utakufa kabisa. Atakuwa ni Mkristo wa jina tu. Bila mahubiri ya Neno la Mungu Wakristo hawawezi kukua katika imani na kumfahamu Yesu Kristo zaidi.

Angalia sana maneno haya ya Efe 4:11-15: "Naye alitoa wengine kuwa . . . manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la *kuwakamilisha watakatifu*, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa *mtu mkamilifu*, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; *ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu*, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo *na kukua hata tumfikie yeye katika yote*, yeye aliye kichwa, Kristo."

Kwa kifupi tunaona hapa kuwa walio Wakristo wanahitaji kuhubiriwa ili wakue katika imani, na ili wasidanganyike na manabii wa uongo na kupoteza imani ya kweli.